# Ufanisi katika Ufundishaji kwenye Shule za Msingi na Sekondari nchini Tanzania

Desemba 2014

hakielimu

## Shukurani

Ripoti hii iliandikwa na Dk. Mkumbo. Ushauri wa kitaalamu ulitolewa na Elizabeth Missokia na Godfrey Boniventura na Florige Lyelu. Pia tunawashukuru Bw. Robert Mihayo na Presscodd James kwa michango yao ya kiuhariri katika ripoti hii.

HakiElimu inatambua michango kutoka kwa walimu na wanafunzi, ambao walitoa michango iliyohitajika kwenye utafiti huu. Shukurani za pekee ziwafikie wakuu wa shule ambao walifanyiwa mahojiano wakati wa utafiti huu pamoja na Wakurugenzi Watendaji wa Wilaya na Maofisa Elimu wa Wilaya ambao waliwaruhusu watafiti kukusanya data kwenye wilaya zao. Tunashukuru kwa ushirikiano na utayari wao kufanya kazi pamoja na sisi.

HakiElimu, 2014

**ISBN 978-9987-18-044-8**

HakiElimu

P.O Box 79401

Dar es Salaam.

Tel:(255 22)2151852/3

Fax: (255 22)21552449

Email: info@hakielimu.org

Website: www.hakielimu.org

Sehemu yoyote ya chapisho hili inaweza kutolewa kwa ajili ya matumizi ya elimu na kwa matumizi yasiyo ya kibiashara, ili mradi tu maelezo yaonesha chanzo na nakala mbili zipelekwe HakiElimu.

## MUHTASARI MAHSUSI

Kwa zaidi ya miongo miwili iliyopita, Tanzania imewekeza sana kwenye sekta ya elimu na matokeo yake yanaonekana katika nyanja nyingi, zinazojumuisha kupanuka kwa kasi kwa sekta ya elimu katika ngazi zote kuanzia elimu ya msingi hadi elimu ya juu. Matokeo yanaonekana hasahasa, katika kuongezeka kwa kasi kwa usajili wa wanafunzi katika ngazi zote. Hata hivyo, kupanuka kwa kasi katika sekta ya elimu kumekuwa hakuendani na uboreshaji wa matokeo ya ujifunzaji. Tafiti nyingi zimekuwa zikifanyika kutathmini matokeo ya ujifunzaji miongoni mwa watoto wa shule na matokeo ya tafiti hizo yanafanana: ingawa watoto wengi zaidi wanahudhuria shule leo kuliko wakati mwingine wowote nchini Tanzania, hawasomi.

Sababu nyingi zimekuwa zikihusishwa na matokeo dhaifu ya ujifunzaji miongoni mwa watoto wa shule, zikijumuisha mazingira dhaifu ya kufundishia na kujifunzia na ukosefu wa nyenzo za kufundishia na kujifunzia. Hata hivyo, kumekuwa na mkazo mdogo kuhusu jinsi matokeo dhaifu ya ujifunzaji yanahusiana na ufanisi katika ufundishaji, ingawa imewekwa sana kwenye maandishi kwamba walimu ni nyenzo muhimu sana katika kuathiri matokeo ya ujifunzaji. Utafiti huu umechunguza kuhusu jinsi matokeo dhaifu ya ujifunzaji miongoni mwa watoto wa shule yanahusiana na ufanisi katika ufundishaji. Swali muhimu lililoongoza utafiti huu lilikuwa: Je, walimu wanafundisha? Utafiti ulifanyika kwenye shule 10 za msingi na shule 10 za sekondari kutoka kwenye wilaya kumi nchini Tanzaniana uliwahusisha zaidi walimu. Data zilikusanywa zaidi zaidi kupitia njia ya kurekodi taarifa za shule na uchunguzi darasani.

Shule zilizoshiriki zilichaguliwa kinasibu na kwa kufuata vigezo maalumu. Uchaguzi nasibu ulitumiwa kwa shule za umma wakati uchaguzi wa kutumia sampuli yenye kufuata kigezo maalumu ilitumika katika kuchagua shule chache za binafsi za sekondari zinazofanya vizuri zaidi. maadhumuni ya kuchagua shule binafsi zinazofanya vizuri zaidi kwa kufuata kigezo maalumu yalikuwa ni kupima mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji na ufanisi katika ufundishaji kwenye shule zinazofanya vizuri zaidi ili kubaini sifa zozote za kipekee zinazozifanya shule hizi kufanya vizuri zaidi kwenye mitihani ya taifa na kuangalia kinachokosekana kwenye shule za umma, ambapo ufaulu wao upo kwenye kiwango cha kati na dhaifu tu. Shule binafsi zilizochaguliwa zilikuwa Shule ya Sekondari ya Wavulana Feza (Dar es Salaam), Shule ya Sekondari ya Wasichana Mariam (Bagamoyo) na Shule ya Sekondari ya Wasichana ya Mtakatifu Fransisko (Mbeya).

Matokeo ya utafiti yanaonesha kwamba shule zinazofanya vizuri zaidi zilikuwa na sifa bainishi nyingi zinazomuhusu mwalimu zikijumuisha:

- Uwiano mdogo kati ya Mwalimu na wanafunzi, ukianzia kati ya 1:8 na 1:26.
- Mahudhurio ya juu ya mwalimu darasani
- Walimu wenye uzoefu wa juu ambao wamefundisha kwa miaka 10 na zaidi. Hii imejidhihirisha kwenye shule za binafsi na baadhi ya shule za serikali hasahasa, shule ya Sekondari Ilboru
- Walimu wenye sifa kwenye masomo yote, wanaoelezewa kama walimu wenye shahada au sifa za juu zaidi
- Walimu walisimamia kazi za wanafunzi darasani kwa ufanisi zaidi
- Walimu waliwasiliana na wazazi mara nyingi na mara kwa mara
- Walimu walitumia Kiingereza mara nyingi darasani. Wakati kwa wastani, asilimia 32 ya walimu walionekana wakitumia Kiingereza kama lugha ya kufundishia wakati wote wa somo, kiwango cha matumizi ya Kiingereza kwenye shule za binafsi kilikuwa asilimia100.
- Walimu walishiriki kwenye kozi za maendeleo ya kitaalamu mara nyingi na mara kwa mara.
- Walimu walitekeleza sana mwongozo wa maadili kwa wanafunzi na ulikuwa unajulikana na ulisambazwa kwa wanafunzi na wazazi.

- Mazingira ya kufundishia, kujifunzia na kuishi yalikuwa yenye kupendeza. Kwa mfano, katika shule za sekondari zilizoonwa walimu walikuwa wakipewa chakula cha bure kafeteria. Walimu pia walikuwa na ofisi nzuri zenye vifaa vyote muhimu vya kufanyia kazi. Kwa kuongezea, walimu walikuwa wakilipwa mishahara mizuri na motisha nyingine (kama vile nyumba, matibabu, n.k). Hali ni tofauti kabisa katika shule za umma na hasa katika shule za kata ambapo walimu walikosa huduma za kuwasaidia kutimiza majukumu yao kwa ufanisi zikijumuisha ofisi. Katika baadhi ya shule, kwa mfano, kutokana na ukosefu wa ofisi za walimu, darasa lilibadilishwa kuwa ofisi ya walimu na bila ya kuwa na samani muhimu. Kwamba mazingira ya kufanyia kazi kwa ujumla yalikuwa mabaya sana kwenye shule nyingi za umma ambayo yaliwakatisha tamaa walimu.

- Bila shaka mchango wa walimu katika shule zinazofanya vizuri zaidi, ulikuwa ni ukweli kwamba walimu katika shule hizo walikuwa wameazimia kufundisha ili wanafunzi waweze kufaulu mitihani. Kwa hakika, kazi yao ina uhusiano na ufaulu mzuri wa wanafunzi. Iwapo wanafunzi wangefanya vibaya, hii ingemaanisha ukomo wa kazi yao katika shule hizi. Kwa kuongezea, uchaguzi wa mwanafunzi kujiunga na shule unafanyika kwa uangalifu sana ambapo ni wanafunzi wenye sifa za juu zaidi huchaguliwa kujiunga na shule hizi. Zaidi zaidi, kuna utaratibu makini wa kuwabakisha wanafunzi, ambapo ni wanafunzi wale tu ambao hufikisha wastani fulani wanaruhusiwa kubaki katika shule na kuendelea na ngazi inayofuata. Kwa mfano, katika mojawapo ya shule binafsi zilizochunguzwa,wanafunzi walilazimika kufikisha wastani wa asilimia 66 katika masomo yote ili kubakia shuleni.

Utafiti pia umeonesha kwamba maandalio ya somo haukuwa utaratibu unaofanana karibu katika shule zote zilizotembelewa. Kwa wastani, ni asilimia55 (51.5%)tu ya walimu walioonwa walikuwa na andalio la somo wakati wa utafiti. Hali ilikuwa inasumbua zaidi katika shule za sekondari za umma ambapo ni asilimia 36.3 tu ya walimu waliochunguzwa walikuwa na maandalio ya somo. Kwa hakika, walimu waliochunguzwa katika shule za binafsi walieleza wazi kwamba andalio la somo lilikuwa halipewi msisitizo katika shule zao bali ufaulu wa wanafunzi katika mitihani.

Kwa kuzingatia matokeo ya utafiti huu, inaweza kuhitimishwa kwamba matokeo ya ujifunzaji wa wanafunzi yana uhusiano mkubwa sana na sababu za wanafunzi kwa mujibu wa takwimu na maelezo. Ufanisi wa walimu ulikuwa unahusiana sana na sifa za walimu, uzoefu, mahudhurio darasani na usimamizi wa kazi za ujifunzaji na tabia za wanafunzi. Kwa ujumla, ufanisi wa walimu ulikuwa ni matokeo ya mazingira ya shule yenye motisha.

Kwa ujumla, ni dhahiri kwamba shule za binafsi na za umma zinaonekana kufanya kazi katika mazingira tofauti ya kufundishia, kujifunzia na kuishi. Pamoja na kwamba utofauti unapaswa kutiliwa mkazo miongoni mwa shule, kunapaswa kuwa na viwango vya chini vya utendaji vinavyopaswa kufikiwa na shule zote. Kwa sasa shule za binafsi zina viwango vyake vya ufaulu , ikijumuisha nani anapaswa kuhudhuria shule hizi. Shule hizi zimeweka taratibu za 'kibaguzi' za kuchagua wanafunzi ili kwamba, mbali na swali kuhusu kiwango cha kipato cha mzazi ni wanafunzi wale tu wenye kipaji wanaruhusiwa kujiunga na shule hizi[1] . ***Kwa kumalizia, kwa hakika aina ya mwalimu haiamui matokeo ya ujifunzaji katika shule binafsi, bali aina ya shule na aina ya watoto wanaochaguliwa kujiunga na shule hizi***.

**Hitimisho**, matokeo ya utafiti huu yanabainisha kwamba ufanisi katika ufundishaji hautofautiani sana kati ya shule binafsi na shule za umma. Matokeo yake, aina ya shule na mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji yanayoambatana na shule husika yanahusika sana katika kuamua ufaulu wa shule kuliko ufanisi katika ufundishaji. Katika kujibu swali lililopo katika utafiti huu kuhusu, Je walimu wanafundisha? Jibu si la moja kwa moja lakini ni dhahiri kwamba ufundishaji katika shule za umma na binafsi zilizoonwa na utafiti huu uko mbali na ufanisi.

Kwa kuongozwa na uchunguzi na hitimisho, inapendekezwa kwamba wananchiwaendelee kusisitiza umuhimu wa mwalimu katika kuboresha ubora wa elimu na kuisukuma Serikali kuendelea kuchukua

1 Kipaji katika muktadha wa utafiti huu kinaelezewa kama wanafunzi wanaofanya vizuri zaidi katika mitihani ya taifa. Wanafunzi hawa kwa kawaida ni wale wanaochaguliwa katika shule za sekondari za serikali (kama vile Ilboru, Mzumbe, Kilakala, Msalato, n.k.).

hatua nyingi za kuboresha ufanisi wa walimu darasani zikijumuisha:

- Kuajiri walimu wengi wenye sifa na kuwapatia motisha kadri inavyowezekana ili wabakie shuleni hasa kwenye shule za vijijini
- Usimamizi wa walimu ili kuhakikisha kwamba wanahudhuria darasani na kufundisha wanafunzi kufuatana na kalenda ya shule
- Kuwamotisha na kuwawezesha walimu kutumia Kiingereza kama lugha ya kufundishia, ambayo kwa sasa inatumika mara chache katika shule za kata za umma. La sivyo, kwa sababu ujifunzaji unaonekana kufanyika katika Lugha ya Kiswahili, Serikali iendelee kupewa 'msukumo' kuingalia upya sera ya lugha katika elimu
- Kuwawezesha walimu kupata fursa ya programu za maendeleo ya kitaalamu, ambayo kwa sasa inaonekana kukosekana katika shule za umma
- Kuwasimamia na kuwahamasisha walimu kufundisha kwa ajili ya kupata maarifa kuliko kufundisha kwa ajili ya kufaulu mitihani kama inavyoonekana kujidhihirisha sasa, hasahasa katika shule za binafsi. Hii inamaanisha pia kuisukuma Serikali kufikiria upya madhumuni na ufanyaji wa mitihani ya taifa. Ni aibu kwamba walimu hawaoni umuhimu wa andalio la somo, ambalo limewekwa kwa mapana yake kama nyenzo muhimu katika kuongoza ufundishaji wenye ufanisi.

# Yaliyomo

**MUHTASARI MAHSUSI** .......... **4**

**ORODHA YA MAJEDWALI NA MICHORO** .......... **8**

**SEHEMU YA I: USULI** .......... **9**

**1.1 UTANGULIZI** .......... 9

**1.2. TATIZO LA UTAFITI** .......... 10

**1.3. MADHUMUNI NA MALENGO YA UTAFITI** .......... 13

**SEHEMU YA II: NJIA YA UTAFITI** .......... **14**

**2.1 AINA NA NJIA** .......... 14

**2.2 SAMPULI NA NJIA ZA KUKUSANYA DATA** .......... 14

2.3 **UCHAMBUZI WA DATA** .......... 15

**SEHEMU YA III: MATOKEO** .......... **16**

**3.1 UTANGULIZI** .......... 16

**3.2 TABIA BAINISHI ZA WALIMU** .......... 16

*3.2.1 Idadi ya walimu na wanafunzi* .......... *16*

*3.2.2 Uzoefu katika ufundishaji* .......... *16*

*3.2.3 Sifa katika ufundishaji* .......... *18*

**3.4 MAZINGIRA YA SHULE KWA UJUMLA** .......... 21

**3.3 MATOKEO KUTOKANA NA UCHUNGUZI DARASANI** .......... 22

*3.3.1 Utangulizi* .......... *22*

*3.3.2 Taarifa za msingi* .......... *22*

*3.3.3 Mazingira ya darasa* .......... *22*

*3.3.4 Upatikanaji wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia* .......... *23*

*3.3.5 Michakato ya ufundishaji na ujifunzaji* .......... *23*

**SEHEMU YA IV: HITIMISHO NA MAPENDEKEZO** .......... **28**

**MAREJEO** .......... **30**

# ORODHA YA MAJEDWALI NA MICHORO


Jedwali la *1: Viwango vya ufaulu katika Kiswahili, Kiingereza na Hisabati katika upimaji uliofanywa kwa kila Wilaya*..................12

Jedwalila 2: *Miaka ya uzoefu katika ufundishaji kwa walimu wa sekondari kila shule*..................17

Jedwali la 3: *Miaka ya uzoefu katika ufundishaji kwa walimu wa shule za msingi kwa kila shule*..................*17*

Jedwali la 4: *Sifa za walimu kwa kila shule (Shule za sekondari)*..................19

Jedwali la 5: *Sifa za walimu kwa kila somo (Shule za sekondari)*..................20

Jedwali la 6: *Sifa za walimu kwa somo (shule za msingi)*..................21

Jedwali la 7: *Kiwango cha Matumizi ya Kiingereza kama Lugha ya Kufundishia katika Shule zilizoonwa*.25

Jedwali la 8: *Uwiano wa walimu walioonesha kuwa wamechukua jitihada kuboresha utendaji wao*..................27


**Michoro**


Mchoro wa *1*: GER na NER katika shule za sekondari nchini Tanzania 2002-2013..................10

*Mchoro wa 2:* Asilimia ya wanafunzi waliofaulu mitihani ya taifa ya Kidato cha IV kati ya mwaka 2000 na 2012..................13

*Mchoro wa 3*: Sifa za walimu kwa shule za msingi na sekondari..................21

*Mchoro wa 4*: Asilimia ya vyumba vya madarasa vilivyoripotiwa kuwa na mazingira ya kujitosheleza ya kufundishia na kujifunzia kwa kundi..................23

*Mchoro wa 5:* Kiwango cha matumizi ya Kiingereza kwa walimu kama lugha ya kufundishia katika madarasa yaliyoonwa..................24

*Mchoro wa 6*: Njia za ufundishaji zilizotumiwa na walimu katika madarasa yaliyoonwa..................25

*Mchoro wa 7*: Kiwango cha kazi za wanafunzi katika madarasa yaliyoonwa..................26

# SEHEMU YA I: USULI

## 1.1 Utangulizi

Tangu mwanzo wa karne hii Tanzania imefanya maendeleo makubwa katika kuhakikisha kuwa idadi kubwa ya watoto wenye umri wa kwenda shule wanapata fursa ya elimu. Hii imewezekana kupitia utekelezaji wa mabadiliko mengi ya sera ya elimu. Mkakati wa kwanza mkubwa wa mabadiliko ya elimu ulianzishwa mwaka 2001 na ulijulikana kama Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM) na ulitekelezwa kwa awamu mbili. Awamu ya kwanza ilitekelezwa kuanzia mwaka 2001 hadi 2006 na mkazo ukiwa kuongeza usajili wa watoto katika elimu ya msingi kupitia ongezeko la rasilimali. Raslimali hizi zilitumiwa kupitia ujenzi wa vyumba vya madarasa, kuajiri walimu wengi , pamoja na kutoa fedha nyingi kwa ajili ya shule (Wizara ya Elimu na Utamaduni [MOEC], 2001).

MMEM uliazimia kufikia elimu kwa wote (UPE) kwa kusajili watoto wote walio na umri wa kati ya miaka7 hadi 13 kwenye darasa la 1 kufikia mwaka 2005. Kuhakikisha kwamba watoto wa masikini wanasajiliwa , serikali iliamua kufuta ada mwaka 2002. Wakati wa utekelezaji wa awamu ya MMEM, kulikuwa na ongezeko kubwa la usajili kwa wavulana na wasichana. Kwa mfano katika mwaka 2002, wakati wa utekelezaji wa awamu ya kwanza ya MMEM, usajili wa darasa la kwanza uliongezeka hadi kufikia asilimia 23.4 . Hadi kufikia mwisho wa mwaka 2002 kulikuwa na watoto zaidi ya milioni moja katika shule za msingi kuliko mwaka 2001 (MOEC, 2003).

Kufikia mwaka 2010, Uwiano wa Jumla wa Usajili (GER)kwa elimu ya msingi ulikuwa 97.6 kwa wavulana na 99.2 kwa wasichana na Uwiano Kamili (NER) ulikuwa 91.4 kwa wavulana na 92.5 kwa wasichana (Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi [MoEVT], 2012). Hii inaonesha kwamba karibu watoto wote walio na umri wa kati ya miaka 7 na 13 walisajiliwa katika shule za msingi. Hata hivyo kasi haikudumu. Uwiano wa wavulana na wasichana katika elimu ya msingi umekuwa ukishuka tangu miaka ya awali ya utekelezaji wa MMEM. Kwa mfano usajili wa wavulana na wasichana mwaka 2012 ulikuwa ni mdogo kuliko mwaka 2009 bali na ongezeko la idadi ya watu. Katika mwaka 2012 kulikuwa na wavulana 4,086,280 katika shule za msingi ukilinganisha na 4,248,764 katika mwaka 2009 na idadi ya wasichana ilishuka kutoka 4,192,789 katika mwaka 2009 hadi 4,160,892 katika mwaka 2012. Hali imeendelea kama inavyooneshwa na data za hivi karibuni za Takwimu za Elimu ya Msingi Tanzania (BEST)(MOEVT, 2014). Kwa ujumla GER na NER zimeshuka kutoka 110.5 na 95.9 katika mwaka 2009 hadi kufikia 98.4 na 92.0 katika kipindi cha 2012 na kufikia 96.2 na 89.7 katika kipindi cha 2013 vilevile, ikiwa inaashiria kwamba kiuwiano kulikuwa na watoto wachache shuleni kuliko awali.

Upungufu katika usajili ni mbaya sana katika baadhi ya mikoa kuliko mingine. Katika mkoa wa Kigoma kwa mfano, watoto 27 kati ya 100 walio na umri wa kwenda shule (7 hadi 13) hawajasajiliwa shuleni. Hata katika mkoa wa Dar es Salaam, watoto 26 kati ya 100 hawapo shuleni. Karibu watoto milioni moja walio na umri wa miaka , 7 hadi 13 hawapo katika shule za msingi nchini kwa sasa. Tatizo linaongezwa zaidi na kiwango kikubwa cha utoro katika shule za msingi. Katika mwaka 2012, kwa mfano, watoto 55,302 waliacha shule kabla ya kumaliza elimu yao ya msingi. Kati ya hao 12,021 miongoni mwao walikuwa darasa la kwanza (MoEVT, 2014). Iwapo hali ya sasa itaendelea , Tanzania haitaonekana kufikia malengo ya milenia ya elimu.

Ongezeko la awali katika usajili liliwezekana kutokana na juhudi kubwa katika ujenzi ambapo vyumba vipya vya madarasa na kwa wakati fulani shule mpya zilijengwa . Serikali pia iliajiri walimu wengi na ilihakikisha kuwa shule zinapatiwa nyenzo za kutosha za kufundishia na kujifunzia.

Katika kujenga kwenye mafanikio ya MMEM, Serikali iliamua kuipeleka programu ya MMEM kwenye programu ya elimu ya sekondari. Kwamba, upanuzi na uboreshaji wa programu ya elimu ya sekondari uliojulikana kama Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari (MMES) ulibuniwa. Huu ulikuwa mpango wa miaka 15 uliotekelezwa katika awamu tatu ukiitwa MMES I, II na III. MMES I ulitekelezwa kati ya mwaka 2004 na 2008 ukiwa na lengo la kupanua upatikanaji wa elimu ya sekondari

kupitia ongezeko kubwa la idadi na vitengo vya shule. Utekelezaji wa MMES II ulianza mwaka 2010 na umeendelea katika mwaka 2014. MMES II inalenga katika kuboresha matokeo ya ujifunzaji hasahasa katika maeneo yasiyostahili.

Kama ilivyokuwa na MMEM, MMES nayo imekuwa na mafanikio katika kupanua upatikanaji wa elimu ya sekondari kupitia ongezeko la idadi ya shule. Hii imesababisha kuwa na na ongezeko la kasi katika usajili wa wanafunzi kutoka 1,222,403 mwaka 2008 hadi kufikia 1,884,272 mwaka 2012 (MoEVT, 2012). Kwa maneno mengine, katika kipindi hiki, uandkikishwaji wa wanafunzi katika elimu ya sekondari umeongezeka kwa zaidi ya asilimia 10 , kutoka asilimia 24.5 mwaka 2008 hadi kufikia asilimia 36.6 na kuifanya Tanzania kuwa nchi ya pili katika idadi kubwa ya usajili Afrika Mashariki ikiifuatia Kenya yenye asilimia 60 (tazama Mchoro namba 1).




| | 2002 | 2003 | 2004 | 2005 | 2006 | 2007 | 2008 | 2009 | 2010 | 2011 | 2012 | 2013 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| GER FORM 1-4 | 9.7 | 10.2 | 12.9 | 15.9 | 20.2 | 30.5 | 36.2 | 43.6 | 47.3 | 50.2 | 51.4 | 45.5 |
| NER FORM 1-4 | 5.9 | 6.3 | 8.4 | 10.3 | 13.4 | 20.7 | 24.4 | 29.1 | 30.8 | 34.5 | 36.6 | 33.7 |
| GER FORM 5-6 | 1.8 | 1.7 | 2.1 | 2.4 | 3.2 | 3.7 | 4.0 | 4.4 | 4.8 | 5.0 | 5.1 | 4.2 |
| NER FORM 5-6 | 0.4 | 0.4 | 0.5 | 0.6 | 1.0 | 0.9 | 1.4 | 1.5 | 1.9 | 2.0 | 2.7 | 1.8 |
| GER FORM 1-6 | 7.1 | 7.4 | 9.4 | 11.7 | 14.8 | 22.1 | 23.5 | 31.3 | 34.0 | 36.1 | 36.9 | 32.1 |
| NER FORM 1-6 | 6.0 | 6.3 | 5.9 | 10.1 | 13.1 | 20.6 | 26.1 | 27.8 | 29.9 | 32.1 | 34.3 | 28.8 |

*Mchoro Namba1*: GER na NER katika shule za seondari nchini Tanzania 2002-2013.

Chanzo: BEST 2014 (2001 hadi 2013)

## 1.2. Tatizo la Kiutafiti

Tanzania, kama inavyoonekana hapo juu, imefanikiwa katika kiwango cha kuridhisha katika kuwasajili watoto wa shule za msingi na sekondari. Kwa kujitoa kwa moyo kwa wadau wote – serikali , wazazi na asasi za kiraia – tatizo la upatikanaji wa elimu linatatulika. Jambo kubwa la kutilia maanani, bila shaka lipo kwenye matokeo ya ujifunzaji. Tafiti mbalimbali zilizofanywa na *Uwezo*[2] kwa watoto wa shule za msingi katika miaka michache iliyopita zinaonesha kwamba matokeo ya ujifunzaji ni dhaifu. Watoto hawapati maarifa na ufahamu ambao walipaswa kuwa wanaupata kama matokeo ya ujifunzaji. Kiwango cha upatikanaji stadi za msingi za kusoma na kufanya hisabati rahisi kipo dhaifu. Maarifa ya kusoma na kufanya hisabati rahisi hutengeneza msingi wa ujifunzaji ambapo bila hayo ujifunzaji zaidi hauwezi kufanyika kwa ufanisi.

2 *Uwezo,* ni jitihada ya miaka mitano inayotekelezwa nchini Kenya, Tanzania na Uganda ikiwa na lengo la kuboresha uwezo katika kusoma na kufanya hisabati miongoni mwa watoto walio na umri wa miaka 6-16 . Tangu mwaka 2009, Uwezo imefanya utafiti mkubwa kitaifa katika kaya kupima usomaji halisi na uwezo katika hisabati kwa watoto walio na umri wa kwenda shule katika nchi tatu.

Tangu mwaka 2009, *Uwezo* imekuwa ikifanya utafiti wa matokeo ya ujifunzaji kwa watoto wa shule za msingi na matokeo yake wakati wote yamekuwa ya kuhuzunisha. Kwa mfano, katika mwaka 2010, watoto karibu 140,000 walipimwa katika wilaya 133 nchini. Uwezo ilipima uwezo wa watoto katika kusoma Kiswahili na Kiingereza na katika hisabati. Majaribio ya *Uwezo* yalijikita katika Mihtasari ya darasa la pili katika masomo matatu ambayo ni Kiswahili, Kiingereza na Hisabati (*Uwezo*, 2011). Muhtasari wa shule za msingi unabainisha kwamba watoto hadi kufikia mwisho wa darasa la pili waweze kusoma matini rahisi katika Kiingereza na Kiswahili na waweze kufanya hisabati rahisi za kujumlisha, kutoa na kuzidisha. Matokeo ya *Uwezo* yanaonesha kwamba katika darasa la 3, ambapo matarajio yalikuwa kwamba watoto wote wangeweza kusoma matini rahisi katika lugha ya Kiswahili, ni theluthi moja tu ya watoto walikuwa na uwezo wa kufanya hivyo. Hadi kufikia darasa la saba, watoto 21 kati ya 100 katika maeneo ya vijijini na 13 kati ya 100 katika maeneo ya mijini walikuwa hawana uwezo wa kusoma matini rahisi ya darasa la pili. Ilikuwa inatisha hasa kwamba watoto 19 kati ya 100 wanaomaliza elimu yao ya msingi kwani walikuwa hawana uwezo wa kusoma na kuandika.

Ingawa idadi kubwa ya watoto wa elimu ya msingi walikuwa hawana uwezo wa kusoma matini rahisi katika Kiswahili , viwango vya usomaji katika Kiingereza vilikuwa chini zaidi. Viwango vya usomaji katika Kiingereza vilikuwa chini zaidi katika madarasa yote. Hakukuwa na tofauti kubwa ya kijinsia katika usomaji wa Kiingereza kwa wanawake na wanaume kuanzia elimu ya awali hadi darasa la 7 wote walikuwa hawafanyi vizuri. Ingawa kusoma Kiingereza ilikuwa changamoto kwa watoto katika mazingira ya mjini na vijijini, watoto wa mijini kwa ujumla walikuwa wakifanya vizuri zaidi ya wale wa vijijini. Kitaifa , zaidi ya asilimia 50 ya watoto wote katika darasa la Saba waliweza kusoma hadithi ya kiwango cha darasa la pili katika lugha ya Kiingereza.

Uwezo ilifanya utafiti mwingine wa kitaifa mwaka 2012. Matokeo katika lugha ya Kiswahili na Kiingereza yalikuwa yanafanana na ufafiti uliofanywa mwaka 2011.Utafiti wa *Uwezo* wa mwaka 2011 na 2012 ulionesha kwamba watoto wachache sana walikuwa wakijifunza kusoma mwanzoni wa shule ya msingi. Kitaifa, ni mtoto mmoja tu kati ya wanne katika darasa la tatu waliweza kusoma hadithi ya kiwango cha Darasa la Pili. Ilikuwa hapana hadi kufikia Darasa la tano ndipo idadi kubwa ya wanafunzi walipoweza kusoma katika kiwango cha Darasa la II. *Uwezo* katika kusoma na kuelewa hadithi katika lugha ya Kiingereza ulibakia chini. Utafiti wa *Uwezo* wa mwaka 2012 umethibitisha kwamba kiwango cha usomaji wa Kiingereza kilikuwa chini zaidi kuliko Kiswahili katika madarasa yote. Kufikia darasa la saba, nusu ya wanafunzi wanaomaliza darasa la saba walikuwa hawana maarifa katika stadi za msingi za kusoma Kiingereza ambayo ni lugha ya mawasiliano katika shule za sekondari.

*Uwezo* pia iliwapima watoto uwezo wao katika stadi za msingi za hisabati. Matokeo ya utafiti yalionesha kwamba utendaji kwa ujumla ulikuwa dhaifu. Kwa mfano, ni asilimia 15 tu ya watoto katika darasa la pili walikuwa na uwezo wa kukokotoa hisabati za kuzidisha. Matokeo ya hisabati yalikuwa mazuri zaidi ya yale ya usomaji. Watoto wengi walionekana kupata stadi za namba baadaye. Viwango vya ufaulu katika majaribio ya hisabati katika mwaka 2012 vilikuwa juu kwa ngazi zote . Kwa mfano asilimia 44 ya wanafunzi katika darasa la 3 walifaulu jaribio la hisabati ukilinganisha na asilimia 37 katika mwaka 2011. Kinachotisha zaidi ni mgawanyiko wa mijini na vijijini kama inavyooneshwa katika Jedwali namba 1.

*Jedwali namba 1: Mifano ya Viwango vya ufaulu katika Kiswahili, Kiingereza na Hisabati katika Wilaya Zilizochaguliwa*

| Wilaya | Kiswahili (%) | Kiingereza (%) | Hisabati (%) | Masomo yote 3 (%) | Kiwango |
|---|---|---|---|---|---|
| Temeke | 74.2 | 45.8 | 80.4 | 66.8 | 1 |
| Arusha Mjini | 64.8 | 55.0 | 78.4 | 66.1 | 2 |
| Morogoro Mjini | 72.3 | 46.2 | 77.8 | 65.4 | 3 |
| Songea Mjini | 68.2 | 51.3 | 75.9 | 65.1 | 4 |
| Kinondoni | 76.1 | 43.6 | 73.8 | 64.5 | 5 |
| Tarime | 17.9 | 12.3 | 43.4 | 24.5 | 122 |
| Biharamulo | 27.0 | 9.2 | 36.3 | 24.2 | 123 |
| Serengeti | 15.4 | 9.5 | 44.7 | 23.2 | 124 |
| Bariadi | 18.8 | 13.9 | 36.1 | 22.9 | 125 |
| Kasulu | 25.3 | 5.7 | 33.0 | 21.3 | 126 |

**Chanzo**: *Uwezo* (2013, 6)

Mbali na eneo ambalo shule inapatikana, ufaulu wa wanafunzi unaendana na kiwango cha elimu cha mama na hali yao ya kijamii-kiuchumi. Watoto ambao mama zao wameelishwa sana wana kawaida ya kufanya vizuri katika usomaji na hisabati. Vilevile watoto kutoka katika familia tajiri hufanya vizuri kuliko watoto kutoka katika familia masikini. Ingawa elimu ya mama na hali yake ya kijamii-kiuchumu huathiri ufaulu katika maeneo yote matatu, athari inaonekana zaidi kwenye Kiingereza (*Uwezo*, 2011).

Matokeo haya huweka changamoto katika sera za nchi za elimu na mipango zinazosisitiza kufikiwa kwa usomaji na stadi za hisabati. Sera ya Elimu na Mafunzo (MoEC, 1995), kwa mfano, inaelezea kwamba madhumuni na malengo ya elimu ya msingi pamoja na mengine ni, "kumwezesha kila mtoto kupata nyenzo za msingi za ujifunzaji kusoma, mawasiliano, stadi za hisabati na utatuzi wa matatizo pamoja na maudhui ya msingi ya ujifunzaji yanayojumuisha elimu inayohusika, ujuzi na mitazamo inayohitajika ili kuishi na maendeleo kuelekea uwezo kamili (uk. 5). MMEM III inaeleza kwamba malengo ya elimu ya msingi "ni kumwezesha kila mtoto kupata ujuzi wa msingi wa kusoma, mawasiliano, stadi za hisabati na utatuzi wa tatizo pamoja na maudhui ya msingi ya ujifunzaji yanayojumuishwa kwenye maarifa yanayohusika na mitazamo inayohitajika ili kuishi na maendeleo kuelekea kwenye uwezo kamili ; kumpatia mtoto misingi inayomwezesha kuwa na jitihada binafsi, kujiendeleza binafsi na kuwa na hali ya kujiamini; kumwandaa mtoto kwa ajili ya ngazi ya pili ya elimu (sekondari,ufundi stadi, ufundina elimu endelevu) na ; kumwandaa mtoto kwa ajili ya ulimwengu wa kazi" (MoEVT, 2012a).

Katika hali inayofanana, ufaulu katika elimu ya sekondari katika mitihani ya umma umekuwa ukishuka katika kiwango cha kutisha tangu kuanzishwa kwa MMES. Kama Mchoro 2 unavyoonesha, ufaulu wa wanafunzi katika mitihani ya taifa ya Kidato cha Nne umekuwa ukishuka na kufikia kiwango cha kutisha katika mwaka 2012 ambapo ni asilimia 34.5 tu ya watahiniwa walifaulu.




*Mchoroe 2:* Asilimia ya watahiniwa ambao walifaulu mitihani ya taifa ya Kidato cha IV kati ya mwaka 2000 na 2012

Swali kubwa linaloikabili sekta nchi nzima ni kwa nini watoto wetu hawajifunzi licha ya raslimali nyingi zinazoelekezwa katika sekta ya elimu, na nini kifanyike kuondokana na mwenendo wa hali ya ufaulu duni?

## 1.3. Madhumuni na malengo ya utafiti

Vigezo vingi huathiri ufaulu wa mwanafunzi. Hivi vinajumuisha kwa mfano, mazingira ya ujifunzaji shuleni (upatikanaji wa vitabu, maktaba, maabara, miundombinu inayoonekana, nk.), maisha ya familia, jamii, mlo, ushiriki katika shughuli zilizo nje ya mtaala, nk. Hata hivyo, ushahidi unaonesha kwamba ufundishaji bora ni kigezo muhimu kuliko vyote katika elimu ya watoto (Fidler, 2002).

Tafiti zinazochunguza sababu zinazoambatana na ufaulu wa mwanafunzi nchini Tanzania kwa kiwango kikubwa zimejikita kwenye uhusiano kati ya mazingira ya ujifunzaji (kama yale yaliyotajwa hapo juu) na matokeo ya ujifunzaji, mkazo mdogo ukiwekwa kwenye sifa bainishi za mwalimu. Kuna tafiti chache kwa hakika ambazo zimechunguza kwa utaratibu unaoeleweka kuhusu jinsi ufanisi katika ufundishaji huathiri matokeo ya ujifunzaji.

Kwa kuzingatia msingi ulioelezwa hapo juu, utafiti huu umedhamiria kuchunguza kwa makini uhusiano uliopo kati ya sifa bainishi za mwalimu na matokeo ya ujifunzaji. Swali kuu linaloshughulikiwa lilikuwa: sifa zipi bainishi za mwalimu ni viashiria vikubwa vya matokeo ya ujifunzaji? Kwa upekee sana, ufanisi katika ufundishaji ulipimwa kwa kuzingatia sifa zifuatazo:

- Uwepo wa mwalimu darasani (mahudhurio ya mwalimu darasani kwa kuzingatia viwango)
- Maandalizi ya mwalimu
- Njia za ufundishaji
- Maarifa ya mwalimu kuhusu somo

# SEHEMU YA II: NJIA YA UTAFITI

## 2.1 Aina na Njia

Utafiti huu umeadhimia kuchunguza ufanisi wa walimu kutokana na mitazamo mingi ikijumuisha uchunguzi wa walimu darasani wakifundisha na vitu vinavyopatikana katika vyumba vya madarasa. Tathmini ya ufanisi wa mwalimu iliongozwa na mwongozo halisi wa ufanisi wa mwalimu uliotengenezwa na Little, Goe na Bell (2009).

Mwongozo halisi wa kutathmini ufanisi wa mwalimu una sifa kuu nne zinazoitwa uchunguzi darasani, tathmini kuu, uchambuzi wa vitu vinavyopatikana darasani, ripoti binafsi ya utendaji kazi na tathmini zinazofanywa na mwanafunzi. Kwa kuendana na mwongozo huu, ufanisi wa mwalimu katika utafiti huu ulipimwa kupitia uchunguzi wa ufundishaji wao na uchunguzi wa vifaa vya ufundishaji na ujifunzaji kama vile uwepo au kutokuwepo kwa nyenzo zinazofanikisha ujifunzaji (michoro, ramani , vitabu, nk.).

Zana tatu zilitumika katika kukusanya data. Zana ya kwanza inahusisha kukusanya sifa bainishi za mwalimu kulingana na idadi ya sifa za mwalimu, ukijumuisha idadi na sifa za walimu, jinsi, uzoefu, mahudhurio darasani na mienendo yenye upungufu. Zana ya pili ilikuwa ni mwongozo wa rekodi ya shule. Zana hii ilikuwa muhimu katika kukusanya data zinazohusiana na sifa za jumla za shule ukijumuisha idadi ya wanafunzi, idadi ya vyumba vya madarasa na nyenzo zingine zinazohusiana (viti, vitabu, nk.), aina ya shule (serikali, binafsi) na mazingira ya jumla ya vyumba vya madarasa na shule. Zana ya tatu ilikuwa orodha ya vitu vya kuchunguza darasani na orodha hii ina vitu vingi vinavyopima vitu vinavyopatikana darasani na shughuli za walimu. Zana hizi zimeambatanishwa kwenye ripoti hii.

## 2.2 Sampuli na njia za ukusanyaji data

Utafiti huu ulifanyika katika wilaya 11 ambazo zilichaguliwa kwa kutumia sampuli nasibu kutoka kwenye kanda zao zinazohusika kama zilivyogawanywa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi. Wilaya hizi ni Kinondoni, Mbeya Mjini, Bagamoyo, Mtwara. Tanga Vijijini, Arusha Vijijini, Singida Vijijini, Tabora Mjini, Mwanza Mjini na Kondoa. Kutoka kwenye kila wilaya shule moja ya sekondari ilichaguliwa kwa kuzingatia kigezo maalumu hasa kwa kuzingatia ufaulu wake katika mitihani ya taifa katika mwaka 2012 yenye ufaulu wa juu, ufaulu wa wastani na ufaulu dhaifu. Zaidizaidi, katika kila wilaya shule moja ya msingi ilichaguliwa kwa kigezo maalumu kwa kuzingatia ukaribu wake na shule ya sekondari iliyoshiriki katika utafiti.

Shule tatu binafsi zilichaguliwa kwa kuzingatia kigezo maalumu katika kupima kigezo cha aina ya mwalimu na mazingira mengine yanayochochea ufaulu wao wa juu na wa kipekee. Shule hizi zilikuwa Shule ya Sekondari ya Wasichana ya Mtakatifu Fransisko (Mbeya), Shule ya Sekondari ya Wavulana Feza (Dar es Salaam) na Shule ya Sekondari ya Wasichana Marian (Bagamoyo). Mtakatifu Fransisko haikushiriki kwa sababu wakati utafiti huu ukifanyika wanafunzi walikuwa wanafanya mitihani ya mwisho wa muhula.

Kwa madhumuni ya uchunguzi darasani masomo matatu yalichaguliwa katika shule za msingi na sekondari. Masomo kwa shule za sekondari yalikuwa Historia, Hisabati na Bailojia. Kwa shule za msingi masomo yalikuwa Hisabati, Sayansi na Stadi za Kazi. Haya ni masomo yenye ufaulu wa chini katika mitihani ya taifa katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita. Mpangilio wenye maelezo ya kina katika shule zilizochaguliwa na vigezo vya uchaguzi vimeoneshwa kwenye mwongozo wa uchunguzi darasani (Kiambatanisho).

Idhini ya kufanya utafiti ilitolewa na Makamu Mkuu wa Chuu Kikuu cha Dar es Salaam, ambapo mtafiti mkuu anafanya kazi kama Profesa Mshiriki. Idhini baadaye ilitumiwa kupata ruhusa ya kufanya utafiti kutoka kwenye mamlaka za wilaya na mkoa ambazo zilitoa ruhusa ya kufanya utafiti katika shule. Kuridhia kwa washiriki kulitafutwa kabla ya wao hawajashiriki kwenye utafiti . Kuridhia kwa wanafunzi kushiriki kwenye utafiti kulipatikana kutoka kwa wakuu wa shule na kwa wanafunzi wenyewe.

Uchunguzi darasani ulifanywa na watafiti ambao walishiriki katika semina ya siku moja ambapo walifahamishwa falsafa na malengo ya utafiti na taratibu za kutumia zana na ujazaji sahihi wa data. Watafiti walitazama madarasa ambapo walimu walikuwa wakifundisha somo katika eneo walilobobea.

## 2.3 Uchambuzi wa data

Data zilizokusanywa katika utafiti huu kwa kiwango kikubwa zilikuwa ni zile zenye asili ya hisabati/takwimu zikiwa na maswali machache yanayomtaka mshiriki kujieleza na ambazo pia zilichambuliwa kwa njia ya maelezo. Data zinazohusisha namba zilichambuliwa kwa kutumia mfumo wa kompyuta na programu ya SPPS na ziliandaliwa katika mfumo wa masafa/frikwensi, majedwali, michoro na njia zingine za kitakwimu.

# SEHEMU YA III: MATOKEO YA UTAFITI

## 3.1 Utangulizi

Utafiti huu umepima ufanisi wa mwalimu kutoka ngazi mbalimbali ambazo zimeoneshwa kwenye sehemu ya njia ya utafiti. Sehemu hii inawasilisha matokeo ya utafiti. Matokeo ya utafiti yamewasilishwa katika sehemu tatu. Sehemu ya kwanza inawasilisha matokeo ya utafiti kuhusu sifa bainishi za mwalimu. Sehemu ya pili inawasilisha matokeo ya utafiti kwa kuzingatia rekodi ya shule, ambayo ilijikita kwenye mazingira ya shule kwa ujumla. Sehemu ya tatu inawasilisha matokeo ya utafiti kwa uchunguzi darasani uliojikita kwenye ufanisi wa mienendo ya walimu katika ufundishaji.

## 3.2 Tabia bainishi za walimu

Kama ilivyoelezwa kwenye sehemu ya njia ya utafiti, utafiti huu ulifanyika katika shule 20, shule 10 zikiwa za msingi na shule 10 zikiwa za sekondari. Sifa bainishi za walimu zilikusanywa kutoka kwenye kila shule na kwa kila somo, ukijumuisha idadi ya wanafunzi, idadi, sifa na uzoefu wa walimu, mienendo yenye upungufu kwa kila sababu na mahudhurio ya mwalimu shuleni na darasani. Katika sehemu hii, tunaelezea sifa hizi.

### 3.2.1 Idadi ya walimu na wanafunzi

Kwa ujumla , shule nyingi zilikuwa na kiwango kinachokubalika cha walimu kukiwa na uwiano wa mwalimu-wanafunzi wa 1:19 kwa shule za sekondari na 1:29 kwa shule za msingi. Hata hivyo, baadhi ya shule zilikuwa na uwiano wa juu zaidi wa mwalimu-wanafunzi ikiwa ni matokeo kwamba zilikuwa na walimu wachache sana. Kwa mfano, Shule ya Sekondari Vihokoli Wilaya ya Mtwara Vijijini ilikuwa na uwiano wa mwalimu-wanafunzi wa 1: 64 na Shule ya Sekondari Hurui iliyopo katika Wilaya ya Tanga Vijijini ilikuwa na uwiano mwalimu-wanafunzi wa 1:49. Kwa hakika, Shule ya Sekondari haikuwa na mwalimu wa somo la Bailojia lakini mwalimu wa somo la Kiingereza alijitolea kufundisha somo hili.Vilevile , kulikuwa hakuna mwalimu wa Hisabati lakini kulikuwa na mhitimu wa Kidato cha Sita aliyekuwa akifundisha somo hili kwa kujitolea.

Sambamba na hilo, shule tatu za msingi zilikuwa na uwiano wa juu kati ya mwalimu na wanafunzi kuliko kiwango cha uwiano unaopendekezwa na Serikali; shule hizi ni Shule ya Msingi Hurui katika Wilaya ya (1:50), Shule ya Msingi Chongoleani katika Wilaya ya Tanga Vijijini (1:94) na Shule ya Msingi Chemchem (1:46). Uwiano wa Mwalimu-wanafunzi unaopendekezwa na Serikali ni 1:40.

Mwenendo huu unaashiria kwamba walimu wengi walikuwa wamejazana katika shule za mjini. Zaidizaidi, shule binafsi zilizotembelewa zilikuwa na uwiano mdogo sana wa mwalimu-mwanafunzi. Kwa mfano, Shule ya Sekondari ya Wavulana Feza iliyopo mkoani Dar es Salam ilikuwa na uwiano wa mwalimu-wanafunzi wa 1:8; Shule ya Wasichana Marian wilayani Bagamoyo 1:26 na Mtakatifu Fransisko mkoani Mbeya 1:16.

### 3.2.2 Uzoefu katika Ufundishaji

Zaidi ya theluthi moja (40%) ya walimu walikuwa na uzoefu katika ufundishaji wa kati ya mwaka mmoja na miaka mitano, na hawa wanaweza kuwekwa katika makundi kama ya wale wasio na uzoefu au wenye uzoefu mdogo. Uwiano wa walimu waliokuwa na uzoefu wa juu zaidi ulikuwa asilimia 22 . Kwa wastani shule binafsi zilikuwa na uwiano wa juu wa walimu wenye uzoefu wa juu zaidi (wakiwa wamefundisha kwa zaidi ya miaka 10 ) kuliko shule za umma. Hata hivyo, Shule ya Sekondari ya Ilboru , shule ya umma inayoko mkoani Arusha, ilikuwa na uwiano wa juu zaidi wa walimu wenye uzoefu(40%) .

Shule za kata zinazopatikana vijijini zilikuwa na uwiano wa juu zaidi wa walimu wasiokuwa na uzoefu, shule ya Sekondari ya Vihokoli iliyopo katika Wilaya ya Tanga Vijijini ilikuwa na uwiano wa juu zaidi wa walimu wasiokuwa na uzoefu (67%), ikifuatiwa na Shule ya Sekondari Chongoleani katika Wilaya ya Mtwara Vijijini iliyokuwa na uwiano wa asilimia 62 ya walimu wasiokuwa na uzoefu(Tazama jedwali 2)

Shule za msingi zilikuwa na uwiano wa juu wa walimu wenye uzoefu kuliko shule za sekondari. Wastani wa uwiano wa walimu wenye uzoefu kati ya walimu wenye uzoefu wa juu ni asilimia 53 . Kama jedwali namba 3 linavyoonesha, ni shule tatu tu zilikuwa na uwiano wa chini ya asilimia 50 ya walimu wasio na uzoefu (inaelezewa kama walimu ambao wamefundisha kwa chini ya miaka kumi).

**Jedwali 2:** ***Uzoefu katika ufundishaji kwa walimu wa shule za sekondari katika asilimia kwa kila shule***




**Jedwali 3:** ***Uzoefu katika ufundishaji kwa walimu wa shule ya msingi katika asilimia kwa kila shule***



### 3.2.3 Sifa katika ufundishaji

Idadi kubwa ya walimu katika shule zilizotembelewa wanaweza kuwekwa katika makundi kama vile wale waliofuzu sana. Kwa mujibu wa Sera ya Tanzania ya Elimu na Mafunzo (URT, 1995), kiwango cha chini cha sifa kwa mwalimu wa sekondari anachotakiwa kuwa nacho ni stashahada katika elimu, na sifa ya kuwa na shahada inachukuliwa kuwa ndiyo sifa bora zaidi. Kwa muktadha wa utafiti huu, walimu wote wenye shahada katika elimu walichukuliwa kama ndiyo waliofuzu zaidi. Kama Jedwali 5 linavyoonesha, kwa wastani, asilimia 71.6 ya walimu walikuwa na shahada katika elimu.

Shule binafsi na shule za umma zilikuwa na uwiano wa juu zaidi wa walimu waliofuzu zaidi. Kwa mfano, walimu wote katika Shule ya Sekondari ya Feza walikuwa wamefuzu na kufikia kiwango cha shahada ya kwanza na zaidi. Asilimia 93 na asilimia 94 ya walimu katika shule ya Sekondari Dk Salmin Amour na Shule ya Sekondari Ilboru vilevile walikuwa na sifa ya kiwango cha shahada ya kwanza na juu ya hapo. Shule za kata zinazopatikana vijijini zilikuwa na uwezekano mkubwa wa kuwa uwiano wa chini zaidi wa walimu waliofuzu zaidi kuliko zile zinazopatikana katika eneo la mjini kama vile Shule ya Sekondari Viholi katika Wilaya ya Mtwara Vijijini.

**Jedwali** ***4: Sifa za Walimu kwa kila Shule (Shule za Sekondari)***

| **Shule** | Shahada | Stashahada | Astashahada | Hakuna sifa | Jumla | %Waliofuzu sana | % Hakuna sifa |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. Marian Wavulana | 34 | 9 | 0 | 0 | 43 | 79 | 0 |
| 2. Dk Salmin Amour | 26 | 2 | 0 | 0 | 28 | 93 | 0 |
| 3. Feza Wavulana | 42 | 0 | 0 | 0 | 42 | 100 | 0 |
| 4. Hurui | 16 | 3 | 0 | 5 | 24 | 67 | 21 |
| 5. Sanjo | 21 | 16 | 0 | 4 | 41 | 51 | 10 |
| 6. Ilboru | 46 | 3 | 0 | 0 | 49 | 94 | 0 |
| 7. Chongoleani | 7 | 4 | 1 | 0 | 12 | 58 | 8 |
| 8. Vihokoli | 2 | 7 | 0 | 0 | 9 | 22 | 0 |
| 9. Tabora Wasichana | 30 | 11 | 3 | 0 | 44 | 68 | 7 |
| 10. Mt Fransisko | 12 | 6 | 0 | 0 | 18 | 67 | 0 |
| **%** | 76 | 20 | 1 | 3 | 100 | | |

Sifa za mwalimu pia zilipimwa kuendana na masomo. Matokeo yameelezwa kwa ufupi katika Jedwali namba 5 na 6. Kwa shule za sekondari, matokeo yanaonesha kwamba, kwa ujumla, idadi kubwa (76%) ya walimu katika masomo mengi walikuwa na sifa ya kiwango cha shahada ya kwanza katika elimu. Hata hivyo, hali ilikuwa tofauti kwa Hisabati ambapo ni walimu kumi tu 10 (46 %) katika somo hili walikuwa na sifa ya kiwango cha shahada ya kwanza, wakati asilimia 41 walikuwa na stashahada katika elimu, na asilimia 13 walikuwa wakifundisha bila ya kuwa na sifa. Baadhi ya shule (Shule ya Sekondari Vihokoli ) haikuwa na mwalimu katika somo la Hisabati, wakati zingine zilikuwa na kati ya mwalimu mmoja tu na wawili (Sanjo, Chongeleani, Dk Salmin Amour na Shule ya Sekondari Hurui ).

Kwa upande wa shule za msingi , matokeo yanaonesha kwamba, kwa ujumla, asilimia 43 ya walimu walikuwa na sifa ya kiwango cha shahada ya kwanza, asilimia 11 walikuwa na stashahada katika elimu na asilimia 44 walikuwa na astashahada katika elimu. Sifa ya msingi kwa walimu wa shule ya msingi ni astashahada katika elimu na stashahada katika elimu inachukuliwa kuwa ni sifa bora kabisa. Jedwali namba 5 linaeleza kwa muhtasari sifa za walimu wa shule za msingi na sekondari.

**Jedwali 5:*Sifa za Walimu kwa kila Somo (Shule za Sekondari)***

| **Somo** | **Shahada na juu ya hapo** | | **Stashahada** | | Astashahada | | Hakuna sifa | | Jumla | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | N | % | N | % | N | % | N | % | N | % |
| 1. Kiswahili | 20 | 61 | 13 | 39 | 0 | 0 | 0 | 0 | 33 | 12 |
| 2. Hisabati | 10 | 46 | 9 | 41 | 0 | 0 | 3 | 13 | 22 | 8 |
| 3. Historia | 37 | 80 | 9 | 20 | 0 | 0 | 0 | 0 | 46 | 16 |
| 4. Jiografia | 27 | 77 | 8 | 23 | 0 | 0 | 0 | 0 | 35 | 13 |
| 5. Bailojia | 21 | 75 | 5 | 18 | 0 | 0 | 2 | 7 | 28 | 10 |
| 6. Kemia | 22 | 85 | 3 | 12 | 0 | 0 | 1 | 3 | 26 | 9 |
| 7. Fizikia | 18 | 69 | 5 | 19 | 0 | 0 | 3 | 12 | 26 | 9 |
| 8. Kiingereza | 32 | 74 | 11 | 26 | 0 | 0 | 0 | 0 | 43 | 15 |
| 9. Uraia | 17 | 81 | 4 | 19 | 0 | 0 | 0 | 0 | 21 | 8 |
| Jumla | 204 | 73 | 67 | 24 | 0 | 0 | 9 | 3 | 280 | 100 |

***Jedwali 6: Sifa za Walimu kwa kila Somo (Shule za Msingi)***

| **Somo** | **Shahada na zaidi** | | **Stashahada** | | **Astashahada** | | **Hakuna sifa** | | **Jumla** | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | N | % | N | % | N | % | N | % | N | % |
| **Kiswahili** | 16 | 41 | 7 | 18 | 16 | 41 | 0 | 0 | 39 | 16 |
| **Hisabati** | 20 | 47 | 3 | 7 | 17 | 39 | 3 | 7 | 43 | 18 |
| **Historia** | 17 | 49 | 2 | 5 | 16 | 46 | 0 | 0 | 35 | 15 |
| **Jiografia** | 15 | 41 | 4 | 10 | 18 | 49 | 0 | 0 | 37 | 15 |
| **Sayansi** | 15 | 38 | 1 | 3 | 21 | 54 | 2 | 5 | 39 | 16 |
| **Kiingereza** | 22 | 46 | 9 | 19 | 16 | 33 | 1 | 2 | 48 | 20 |
| Jumla | 105 | 44 | 26 | 62 | 104 | 44 | 6 | 2 | 241 | 100 |




*Mchoro3*: Sifa za Walimu kwa Shule za Msing na Sekondari

## 3.4 Mazingira ya Shule kwa Ujumla

Kabla ya uchunguzi darasani, watafiti walifanya uchunguzi wa rekodi ya shule ili kupima mazingira ya shule kwa ujumla. Madhumuni ya zoezi hili yalikuwa kupima ni kwa namna gani miktadha ya shule iliwezesha au ilikuwa kikwazo katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji.

Kwa ujumla , miundombinu inayoonekana ya shule nyingi zilizotembelewa ilikuwa katika hali mbaya ikiambatana na uchafu na kuta zilizopasuka na sakafu zisizo na saruji na vyumba vya madarasa vikiwa na upitishaji dhaifu wa hewa. Katika baadhi ya shule, kulikuwa na vyumba vitano tu vya madarasa ambapo mojawapo ya chumba kilitumika kama bweni la wanafunzi. Katika shule nyingi za kata za umma hakukuwa na ofisi za walimu na walimu walilazimika kutumia viti na madawati ya wanafunzi.

Hata hivyo, hali ilikuwa tofauti sana katika shule binafsi, kama vile Shule ya wavulana Feza na Shule ya Sekondari ya Wasichana Marian . Mazingira ya jumla ya shule na vyumba vya madarasa katika shule hizi ni mazuri sana kwa mwonekano na kwa madhumuni ya kitaaluma. Katika vyumba vyote vya madarasa , kuna mashelfu ya vitabu yaliyotunzwa vizuri na kuna kamera katika kila korido ili kusimamia mahudhurio darasani. Ofisi za walimu zipo katika mazingira mazuri sana, zimetunzwa vizuri na zina samani zinazohitajika. Huduma zote muhimu zinapatikana, kama vile umeme, maji, Kafeteria na huduma na afya. Zaidizaidi, kuna maabara na maktaba nzuri.

## 3.3 Matokeo ya Utafiti unaotokana na uchunguzi darasani

### *3.3.1 Utangulizi*

Madhumuni ya uchunguzi darasani yalikuwa ni kupima ufanisi katika shughuli za ufundishaji kwa walimu na mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji. Uchunguzi darasani uliongozwa na orodha ya mambo ya kuchunguza darasani yaliyochukuliwa kutoka kwenye zana nyingi za uchunguzi darasani ambazo zimeidhinishwa na kujaribiwa katika miktadha mbalimbali. Orodha ilikuwa na jumla ya vitu 65 vilivyogawanywa katika sehemu kuu nne, zinazojulikana kama taarifa za msingi, mazingira ya darasa, upatikanaji wa vifaa vya ujifunzaji na michakato ya ufundishaji na ujifunzaji. Matokeo yamewasilishwa kulingana na mgawanyo huu.

### 3.3.2 Taarifa za msingi

Taarifa za msingi zilizokusanywa wakati wa uchunguzi zilijumuisha jina la wilaya na shule, masomo yaliyochunguzwa, viwango vya darasa, tarehe, majina ya walimu na taarifa zao za kidemografia (jinsi, umri, sifa, uzoefu), tarehe ya uchunguzi na jina la mchunguzi (mtafiti), pamoja na mahudhurio darasani.

Jumla ya vipindi 55 vya uchunguzi darasani vilifanyika. Madarasa yaliyochunguzwa yanajumuisha Sayansi (18.2%), Bailojia (18.2%), Hisabati (27.3%), Stadi za kazi (12.7%) na masomo yanayohusiana na stadi za watu na sanaa (23.65). Hii maana yake ni kwamba jumla ya walimu 55 walionwa wakati wakifundisha, ambapo asilimia 65.5 walikuwa walimu wa kiume na asilimia 34.5 walikuwa walimu wa kike.

Madarasa yaliyochunguzwa yalikuwa Vidato vya I, II, III na IV kwa shule za sekondari na Darasa la V, VI na VII kwa shule za msingi.

Kwa kuzingatia mahudhurio darasani, idadi kubwa ya walimu walihudhuria madarasa yaliyopangwa kufuatana na ratiba. Kwa shule za msingi, wastani wa mahudhurio ulikuwa asilimia 87 na kwa shule za sekondari wastani wa mahudhurio ulikuwa asilimia 89 . Kiwango cha mahudhurio kilikuwa cha juu zaidi miongoni mwa walimu wa shule za sekondari za binafsi zikiwa na wastani wa mahudhurio wa asilimia 100 . Kiwango cha chini zaidi cha mahudhurio kilikuwa katika Shule ya Sekondari Sanjo (27%, N=11), Shule ya Sekondari Chongoleani (27%, N=15) na Shule ya Sekondari Vihokoli(50%, N=6).

### *3.3.3 Mazingira ya Darasa*

Ubora wa mazingira ya shule ulipimwa kwa kuzingatia sifa kuu saba zinazojulikana kama nafasi ya kutosha ya kukaa, nafasi ya kutosha ya kuandikia kwa ajili ya wanafunzi, upatikanaji wa viti na meza kwa walimu, mwanga wa kutosha, upitishaji wa hewa na joto, mazingira ya vyumba vya madarasa na sakafu yenye kufurahisha. Matokeo yameelezwa kwa muhtasari katika Mchoro na Jedwali hapo chini.

Kwa ujumla mazingira yalikuwa yenye kutosheleza katika ujifunzaji ambapo zaidi ya theluthi mbili ya vyumba vya madarasa vilivyoonwa vilikuwa na mazingira ya kutosheleza ya ujifunzaji, mbali na vigezo vya viti na madawati ya walimu. Asilimia 53 tu ya vyumba vya madarasa vilivyoonwa vilikuwa na viti na madawati yaliyoandaliwa kwa ajili ya walimu.




*Mchoro 4*: Madarasa yaliyoripotiwa kuwa na mazingira yanayojitosheleza kwa ajili ya kufundishia na kujifunzia kwa kila kundi katika asilimia

### *3.3.4 Upatikanaji wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia*

Watafiti walihitajika kuchunguza upatikanaji wa baadhi ya vifaa muhimu vya kufundishia na kujifunzia darasani. Hivi vilijumuisha upatikanaji wa vitabu vya kiada, madaftari, ubao na vifaa vinavyohusiana (dasta, chaki) na zana za kufundishia zinazoonekana. Matokeo ya utafiti yanaonesha kwamba nyenzo za kufundishia zinazotumika zaidi zilikuwa vitabu, madaftari na ubaona vifaa vinavyohusiana na hivyo, ambapo zaidi ya asilimia 80 ya madarasa yaliyoonwa yalikutwa yakizitumia.

Chati za ukutani na zana za kufundishia zinazoonekana zilikuwa hazitumiki sana katika michakato ya kufundishia na kujifunzia katika madarasa yaliyoonwa. Kwa mfano, chini ya asilimia10 (7.3%) ya madarasa yaliyoonwa yalikutwa yakiwa na chati za ukutani. Sambamba na hilo, yaani karibu na robo (23.6%) ya madarasa yaliyoonwa yalikuwa na walimu waliokuwa wakitumia zana za kufundishia za kuona. Hali hii haikuwa ya kipekee katika shule binafsi zilizoonwa.

### 3.3.5 Michakato ya ufundishaji na ujifunzaji

Sehemu hii inajumuisha nyanja mbalimbali katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji, kuanzia kwenye maandalizi hadi katika upimaji wa matokeo ya ujifunzaji. Kwamba, nyenzo za maandalizi ya mwalimu na kazi vilipimwa kabla ya kuchunguzwa katika mazingira halisi ya ufundishaji. Katika sehemu hii, tunawasilisha matokeo kwa kuzingatia sehemu mbalimbali za uchunguzi uliofanywa darasani katika michakato ya ufundishaji na ujifunzaji.

#### *3.3.5.1 Maandalizi ya mwalimu*

Maandalizi ya ufundishaji huanza na maandalio ya somo. Kwa mantiki hii, watafiti walichunguza iwapo mwalimu alikuwa na andalio la somo na kwa jinsi gani lilikuwa na ufanisi katika kujibu mada husika zinazofundishwa. Kwa ujumla, katika walimu 55 walioonwa, ni asilimia 51.5 ndio walikuwa na andalio la somo. Walimu wa shule za msingi walionekana zaidi kuandaa andalio la somo kuliko walimu wa shule za sekondari; asilimia 66.7 ya walimu wa shule za msingi walioonwa walikuwa na andalio la somo ukilinganisha na asilimia 36.3 tu ya walimu wa shule za sekondari walioonwa.

Uchunguzi wa makini wa maandalio ya somo yaliyoonwa unaonesha kwamba chini ya nusu (43.6%) ya haya yalikuwa na malengo yaliyokuwa yakionesha waziwazi shuguli za wanafunzi kuliko shughuli za walimu. Zaidizaidi, chini ya theluthi (29.2%) ya andalio la somo lilikuwa na kazi za wanafunzi katika somo lililofundishwa.

### *3.3.5.2 Matumizi ya vitabu vya kiada na lugha ya kufundishia*

Matumizi ya vitabu vya kiada vilivyopo kwa wanafunzi na na matumizi ya lugha sahihi/inayofaa ya kufundishia kwa walimu vilipimwa kama kama kigezo muhimu katika ufanisi wa ufundishaji. Matokeo yanaonesha kwamba, kati ya madarasa 55 yaliyoonwa, ni theluthi moja tu (36.7%) ya wanafunzi walikuwa wakitumia vitabu vya kiada vinavyopatikana darasani. Zaidizaidi, matokeo yanaonesha kwamba, kwa shule za msingi, walimu walitumia Kiswahili (lugha ya kufundishia katika shule za msingi (93.4%) katika kipindi chote cha somo. Hata hivyo, kwa shule za sekondari, Kiingereza (lugha ya kufundishia katika shule za sekondari) ilikuwa ikitumika kama lugha ya kufundishia mara chache ikiwa ni asilimia 31.5 tu ya masomo yaliitumia muda wote (tazama Mchoro 5).

Kulikuwa na utofauti mkubwa wa matumizi ya Kiingereza kama lugha ya kufundishia katika shule za sekondari zilizoonwa. Shule binafsi zilikuwa na kawaida ya kutumia Kiingereza mara nyingi kuliko shule za umma. Shule za umma za kata zilitumia Kiingereza mara chache kuliko shule zingine (tazama Mchoro 6).




*Mchoro5:* Kiwango cha matumizi ya Kiingereza kama lugha ya kufundishia kwa walimu katika madarasa yaliyoonwa

**Jedwali 6:*Kiwango cha Matumizi ya Kiingereza kama lugha ya kufundishia katika shule zilizoonwa***

| | | *Muda wote* | *Karibu 3/4* | *Karibu 1/2 Au chini* |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Shule ya Sekondari Feza Wavulana | 100 | - | - |
| 2. | Shule ya Sekondari ya Wasichana Marian | 100 | - | - |
| 3. | Shule ya Sekondari Dk Salmin Amour | 67 | 33 | - |
| 4. | Shule ya Sekondari Sanjo | - | 40 | 60 |
| 5. | Shule ya Sekondari Ilboru | 33 | 67 | - |
| 6. | Shule ya Sekondari Changoleani | - | - | 100 |
| 7. | Shule ya Sekondari Vihokoli | - | 40 | 60 |
| 8. | Shule ya Sekondari ya Wasichana Tabora | - | 100 | - |
| 9. | Shule ya Sekondari ya Hurui | - | 40 | 60 |

### *3.3.5.3 Uelewa wa Walimu katika mada*

Kwa ujumla , uelewa wa walimu katika mada ulikuwa wa juu sana. Kati ya walimu 55 walioonwa, asilimia 94.5 waliwekwa kama wenye uelewa wa juu kuhusu somo walilokuwa wakifundisha. Hakukuwa na tofauti kubwa katika shule kuhusu uelewa wa walimu kuhusu mada.




*Mchoro 6*: Njia za kufundishia zilizotumiwa na walimu katika madarasa yaliyoonwa

### *3.3.5.4Njia za Kufundishia*

Kwa madarasa mengi yaliyoonwa, njia kuu za kufundishia zilikuwa ni mihadhara na vipindi vya maswali na majibu ikiwa ni karibu robo ya walimu katika madarasa yaliyoonwa walikuwa wakitumia njia hizi. Kwa madarasa mengi, ushiriki wa wanafunzi haukuwa wa mara kwa mara. Kwa mfano, chini ya asilimia 10 (9.1%) katika madarasa yaliyoonwa yalikuwa na wanafunzi waliokuwa wakifanya kazi katika vikundi na ni asilimia 11.1 ya madarasa yaliyoonwa yalikuwa na walimu waliokuwa wakijibu maswali ya wanafunzi. Karibu hakuna walimu walioonwa (1.9%) waliokuwa wakifanya kazi pamoja na wanafunzi, hii ikiashiria kwamba walimu hawashughulikii mahitaji mahsusi ya mwanafunzi mmojammoja ya wanafunzi wao katika mchakato wa ujifunzaji. Hii inaashiria pia kwamba mchakato wa ufundishaji bado kwa kiwango kikubwa unaegemea kwa mwalimu ingawa mtaala unasisitiza katika kutumia njia ambazo zinamtumia mwanafunzi kama msingi mkuu wa ujifunzaji.

### *3.3.5.5Kazi za wanafunzi*

Kazi za wanafunzi ni kigezo muhimu katika ufundishaji na ujifunzaji. Katika utafiti huu kazi nyingi za wanafunzi zilipimwa kuchunguza kiwango cha ushiriki wa wanafunzi katika michakato ya ufundishaji na ujifunzaji. Matokeo yameelezwa kwa muhtasari katika Mchoro 7. Kama mchoro huu unavyoonesha, kuandika (74.5%) na kujibu maswali (76.4%) ndivyo vilivyotawala katika kazi za wanafunzi. Kazi nyingine kama vile kuchora, kutatua matatizo, kusoma au kuuliza walimu maswali zilionekana mara chache. Hii inadhihirisha kwamba michakato ya ufundishaji na ujifunzaji katika shule zilizoonwa kwa kiwango kikubwa ziliegemea upande wa mwalimu.




*Mchoro7*: Kiwango cha kazi za mwanafunzi katika madarasa yaliyoonwa

### *3.3.5.6Utaratibu wa Maadili*

Usimamizi wa darasa ni miongoni mwa vigezo muhimu katika kufanikisha ufundishaji na ujifunzaji. Hii inaakisiwa kwa kiwango kikubwa na utaratibu wa maadili shuleni na katika ngazi ya darasa. Inashauriwa kwamba utaratibu wa maadili katika shule na darasani uwekwe sehemu inayoonekana na ufahamike kwa wanafunzi wote na wafanyakazi.Katika utafiti huu, tulichunguza upatikanaji wa utaratibu wa maadili uliowekwa sehemu ya wazi kwa wanafunzi kuona na aina ya utaratibu wa kinidhamu.

Matokeo yanaonesha kwamba shule zote binafsi zilizotembelewa (Shule ya wavulana Feza na Shule ya wasichana Marian ) wameweka utaratibu wa maadili ulioandikwa lakini vitu hivi vilikuwa havijawekwa popote katika katika mazingira ya shule na milango ya vyumba vya madarasa. Badala yake taratibu za maadili zilikuwa zimewasilishwa kwa wazazi wote mara kwa mara. Kwa shule za umma, utaratibu wa maadili uliwasilishwa katika utaratibu wa dharura na mambo ya maadili hayakuwa yamewekwa kwa namna yoyote.

Mkakati uliozoeleka sana wa kuwaadhibu wanafunzi wenye utovu wa nidhamu ulikuwa ni kuwafokea ikifuatiwa na kuwapiga. Hata hivyo, tabia za utovu wa nidhamu zilionekana mara chache wakati wa kipindi cha utafiti.

### *3.3.5.7 Uchunguzi Mwingine*

Maswali mengine matatu yanayoendana na ufanisi katika ufundishaji yalichunguzwa. Haya ni: je mwalimu ana utaratibu wa mara kwa mara wa kufuatilia iwapo mwanafunzi amemaliza kazi? Je mwalimu huwasiliana mara kwa mara na familia kuhusu maendeleo ya wanafunzi? Je mwalimu hushiriki mara kwa mara katika kozi za maendeleo ya kitaaluma kama vile semina, warsha? Matokeo yameelezwa kwa muhtasari katika Jedwali 8.

Kama Jedwali 8 linavyoonesha, walimu katika shule binafsi walikuwa na utaratibu uliopangika vizuri kusimamia kazi za wanafunzi, walikuwa wakiwasiliana na familia mara nyingi na walishiriki katika kozi za maendeleo ya kitaalamu mara kwa mara kuliko walimu wa shule za umma.

**Jedwali 7:** *Uwiano wa Walimu wa Sekondari ambao walibainisha kuchukua Jitihada Mbalimbali kuboresha utendaji wao*:

| | % Walimu wenye utaratibu wa mara kwa mara wa kufuatilia ukamilifu wa kazi anazopewa mwanafunzi | Walimu mara kwa mara huwasiliana na familia kuhusu maendeleo ya mwanafunzi | Walimu hushiriki mara kwa mara katika kozi za maendeleo ya kitaalamu |
|---|---|---|---|
| 1. Shule ya Sekondari ya Wavulana Feza | 100 | 100 | 100 |
| 2. Shule ya Sekondari ya Wasichana Marian | 100 | 100 | 66.7 |
| 3. Shule ya Sekondari Dk Salmin Amour | 66.7 | 0 | 0 |
| 4. Shule ya Sekondari Sanjo | 40 | 20 | 20 |
| 5. Shule ya Sekondari Ilboru | 66.7 | 66.7 | 33.3 |
| 6. Shule ya Sekondari Changoleani | 50 | 100 | 0 |
| 7. Shule ya Sekondari Vihokoli | 33.3 | 0 | 0 |
| 8. Shule ya Sekomdari ya Wasichana Tabora | 100 | 50 | 100 |
| 9. Shule ya Sekondari Hurui | 66.7 | 0 | 0 |

## SEHEMU YA IV: HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

Utafiti huu ulipima ufanisi wa walimu kutokana na sifa kuu nne ambazo ni mahudhurio darasani, maandalizi, njia za kufundishia na ufahamu wa walimu kuhusu mada ambayo wamepewa kazi ya kufundisha.

Matokeo yanaonesha kwamba mahudhurio darasani kwa walimu kwa ujumla yalikuwa ya juu ikiashiria kuwa idadi kubwa ya walimu katika shule nyingi huhudhuria vipindi kulingana na viwango na miongozo iliyowekwa. Hata hivyo, matokeo pia yanabainisha taswira inayosumbua katika baadhi ya shule ambapo kiwango cha mahudhurio darasani kwa mwalimu kiko chini kama asilimia 27 ikiashiria kwamba chini ya theluthi ya walimu walihudhuria madarasa yaliyopangwa. Hii hasahasa ilikuwa ikionekana katika shule za umma za kata ambazo zinapatikana katika wilaya za vijijini.

Matokeo ya utafiti yanaonesha kwamba idadi kubwa ya walimu hawajaandaliwa vizuri kufundisha kama ilivyoonekana kwa kukosa andalio la somo, ambalo linachukuliwa kuwa zana muhimu na ushahidi wa maandalizi ya mwalimu katika kufundisha. Hii inatoa jibu kwamba ufundishaji wao hauna mpangilio na usioweza kukabili vizuri matokeo ya ujifunzaji kama yalivyopangwa katika mihtasari mbalimbali ya somo. Hii inaweza kuthibitishwa zaidi na matokeo mengine ya utafiti huu yanayoonesha kwamba njia ya kufundishia katika shule zilizoonwa iliegemea zaidi kwa upande wa mwalimu na ushirikishwaji wa wanafunzi ulikuwa mdogo. Hii pia inaoneshwa kwa kutawala kwa matumizi ya mhadhara kwa walimu kama njia za kufundishia na na mawasiliano na ushirikishwaji wa wanafunzi ukiwa mdogo. Kwa uwazi zaidi, kwa hiyo, aina ya ufundishaji wa walimu kwa kiwango kikubwa haiendani na falsafa ya mtaala unaojenga uwezo, ambao unasisitiza mwanafunzi kuwa msingi wa ufundishaji.

Ufahamu wa walimu kuhusu mada katika madarasa yaliyoonwa unaweza kuelezewa kama wenye kujitosheleza. Idadi kubwa ya walimu walionekana kumudu maeneo yao ya ufundishaji kwa kuwa walikuwa na uwezo wa kuridhisha. Hata hivyo, uwasilishaji wa maudhui ulikuwa umeparaganyika sana kutokana na udhaifu katika kuimudu lugha ya Kiingereza kama lugha ya kufundishia katika shule za sekondari. Kwa sababu ya udhaifu katika kuimudu lugha ya mawasiliano, idadi kubwa ya walimu waliamua kutumia Kiswahili katika sehemu kubwa ya ufundishaji wao.

Kwa muhtasari, matokeo yanabainisha kuwa shule zenye ufaulu wa juu zilikuwa na sifa bainishi kumi zifuatazo:

- Uwiano mdogo kati ya mwalimu-wanafunzi
- Mahudhurio ya juu ya mwalimu darasani
- Uwiano wa juu wa walimu wenye uzoefu wa juu sana, wakiwa wamefundisha kwa miaka 10 na zaidi.
- Uwiano wa juu wa walimu wenye sifa zaidi katika masomo yote, wanaoelezewa kama walimu wenye shahada ya kwanza na sifa za juu zaidi
- Usimamizi wa karibu wa walimu
- Walimu walikuwa wakiwasiliana na wazazi mara nyingi na mara kwa mara
- Walimu walitumia Kiingereza mara nyingi darasani.
- Walimu walishiriki katika kozi za maendeleo ya kitaalamu mara nyingi na mara kwa mara.
- Walimu walitekeleza kwa makini utaratibu wa maadili kwa wanafunzi ambao ulikuwa ukifahamika kwa wengi na ulisambazwa kwa wanafunzi na wazazi.
- Mazingira ya ufundishaji, ujifunzaji na kuishi yalikuwa yenye kuvutia na kutia motisha kama yalivyojiakisi katika upatikanaji wa chakula shuleni, ulipaji wa mshahara kwa wakati na upatikanaji wa motisha kwa mwalimu (kama vile nyumba na huduma za matibabu), upatikanaji wa vitendea kazi kwa mwalimu kama vile ofisi na vitendea kazi vinavyofanana na hivyo.

Kwa ujumla, ni dhahiri kwamba shule za umma na zile za binafsi zinaonekana kufanya kazi katika mazingira tofauti kabisa ya kufundishia, kujifunzia na kuishi. Pamoja na kwamba utofauti unapaswa kuhamasishwa miongoni mwa shule, ni lazima kuwa na viwango vya chini vya utendaji wa kazi ambavyo vinapaswa kufikiwa na shule zote. Kwa sasa shule binafsi zina viwango vyao vya utendaji vikijumuisha ni nani anapaswa kuhudhuria katika shule hizi. Shule hizi zimeweka taratibu za 'kibaguzi' sana katika kuchagua wanafunzi ili kwamba, mbali na swali kuhusu uchumi wa wazazi, ni wale tu watoto wenye vipaji[3] wanaruhusiwa kujiunga na shule hizi. ***Kwa kumalizia kusema kweli siyo aina ya mwalimu tu ndiyo huamua matokeo ya ujifunzaji katika shule binafsi, bali aina ya shule na aina ya watoto wanaochaguliwa kujiunga na shule hizi***. Kwa kuhitimisha, matokeo ya utafiti huu yameonesha kwamba ufanisi katika ufundishaji hautofautiani sana kati ya shule binafsi na shule za umma. Kwamba, aina ya shule na mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji yanayopatikana katika shule husika ni ya msingi sana katika kuamua ufaulu wa shule kuliko ufanisi katika ufundishaji. Katika kujibu swali lililopo katika utafiti huu, linalojulikana kama Je walimu wanafundisha? Jibu si la moja kwa moja bali ni dhahiri kwamba ufundishaji katika shule za umma na binafsi ulioonwa katika utafiti huu uko mbali na kuwa wenye kuleta ufanisi.

Matokeo na hitimisho katika utafiti huu vinapaswa kuchukuliwa kwa uangalifu. Hii ni kwa sababu ni shule chache tu ndizo zilihusishwa katika utafiti huu. Kwa kuongezea, katika shule tatu za binafsi ambazo zimekuwa zikifanya vizuri katika mitihani ya taifa zilichaguliwa kwa makusudi ili kuonesha baadhi ya mazingira ya ufundishji na ujifunzaji ambayo yanaweza kuwa yenye kufanikisha zaidi katika kukuza matokeo ya ujifunzaji. Kwa hakika, matokeo na hitimisho vinaweza visitoe taswira inayowakilisha utendaji wa walimu kitaifa. Kwa kuongezea, aina ya shule binafsi zilizochaguliwa kwa ajili ya utafiti huu zinaweza zisiwakilishe shule nyingi za binafsi nchini ambazo mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji pia ni duni na kwa kiwango kikubwa yanaweza kulinganishwa na shule nyingi za umma.

Kwa kuzingatia uchunguzi na hitimisho lililopo hapo juu, inapendekezwa kwamba wananchi waendelee kutilia mkazo umuhimu wa walimu katika kuboresha ubora wa elimu, na kuisukuma Serikali ili iendelee kuchukua hatua mbalimbali za kuboresha ufanisi wa walimu madarasani, zikijumuisha:

- Kuajiri walimu wengi wenye sifa na kuwamotisha ili wabakie shuleni hasa kwenye shule zilizo katika maeneo ya vijijini na kufanya kazi kwa bidii ili kuleta mabadiliko chanya.
- Kuwasimamia walimu ili kuhakikisha kuwa wanahudhuria darasani na kuwafundisha wanafunzi kulingana na ratiba ya shule na mipango ya kazi.
- Kuwamotisha na kuwawezesha walimu kutumia Kiingereza kama lugha ya kufundishia. Hili kwa sasa linafanyika mara chache katika shule za umma za kata. La sivyo, kwa sababu ujifunzaji unaonekana kufanyika katika lugha ya Kiswahili, Serikali iendelee kupewa 'msukumo' kuiangalia upya sera ya elimu kuhusu lugha.
- Kuwawezesha walimu kupata programu za maendeleo ya kitaalamu, ambazo zinaonekana kukosekana katika shule za umma
- Kuwasimamia na kuwahamasisha walimu kufundisha kwa ajili ya kujifunza kuliko kwa ajili ya kufaulu mitihani kama inavyoonekana kuwa ndiyo utaratibu wa sasa hasa katika shule binafsi. Hii inaweza kujumuisha kuwasimamia walimu kujipanga kwa umakini na kufundisha kulingana na matokeo ya ujifunzaji yaliyopangwa katika mihtasari ya masomo mbalimbali na mtaala. Ni aibu kwamba walimu hawaoni umuhimu wa andalio la somo katika ufundishaji, ambalo limewekwa kwa kiwango kikubwa kama nyenzo muhimu katika kuongoza ufundishaji wenye ufanisi.
- Kuisukuma Serikali kufikiria upya kuhusu madhumuni na matumizi ya mitihani ya taifa kama njia ya tathmini ya mwisho kwa wanafunzi.

---

3 Kipaji katika muktadha wa utafiti huu kinaelezewa kama wanafunzi wanaofanya vizuri zaidi katika mitihani ya taifa. Wanafunzi hawa ambao kwa kawaida huchaguliwa katika shule za sekondari za serikali zilizoteuliwa (kama vile Ilboru, Mzumbe, Kilakala, Msalato, nk.).

## MAREJEO

Fidler, P. (2002). *The relationship between teacher instructional techniques and characteristics and student achievement in reduced size classes.* CA: Los Angeles Unified School District, Programme Evaluation and Research Branch. Retrieved from http://files.eric.ed.gov/fulltext/ED473460.pdf

URT (1995) **Education and Training policy** Dar es Salaam: Ministry of Education and Culture

URT (2001) **Education Sector Development Programme: Primary Education Development Plan (2002 – 2006),** Dar es Salaam:Basic Education Development Committee (BEDC), Ministry of Education and Culture.

URT (2003) 'Education Sector Public Expenditure Review 2003' Dar es Salaam: Ministry of Education and Culture.

URT (2012) **Basic Education Statistics in Tanzania (BEST) 2008 – 2012 National Data** Dar es Salaam: Ministry of Education and Vocational Training

URT (2012a) "Primary Education Development Programme III" Basic Education Development Committee, Ministry of Education and Vocational Development.
URT (2013) **MpangowaMatokeoMakubwaSasaSektayaElimu** Dar es Salaam: WizarayaElimunaMafunzoyaUfundi

URT (2014) **Basic Education Statistics in Tanzania (BEST) 2009 – 2013 National Data (Draft)** Dar es Salaam: Ministry of Education and Vocational Training

Uwezo (2011) **Are our Children Learning? Annual Learning Assessment Report** Dar es Salaam: Uwezo Tanzania.

Uwezo (2013) **Are our Children Learning? Annual Learning Assessment Report** Dar es Salaam: Uwezo Tanzania.

**Ufanisi katika Ufundishaji kwenye Shule za Msingi na Sekondari nchini Tanzania**

hakielimu

S. L. P. 79401, Dar es Salaam, Tanzania
Simu: +255 (22) 2151852 au 3
Nukushi: +255(22) 2152449
Barua pepe: info@hakielimu.org
Tovuti: www.hakielimu.org